

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**

SHULE YA SEKONDARI MAGU,  
S.L.P 186,  
MAGU.

**MOB 0754-912801/0762-025831**  
TAREHE 15/12/2020

**Kumb Na MSS/VOLI/F1/04**

**Jina la Mwanafunzi.....**

**S.L.P.....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA  
SEKONDARI MAGU WILAYA YA MAGU MKOA WA MWANZA MWAKA  
2021**

**1.0 Utangulizi**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, **Shule ya Sekondari MAGU** ipo umbali wa **Km Mbili (2)** Magharibi mwa Halmashauri ya **MAGU**.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 (Baada ya tarehe 25/01/2021 hutapokelewa).

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1 Sare za Shule**

**a). WASICHANA**

- i. Sketi mbili (2) rangi ya Dark Blue, ndefu inayofika kwenye kifundo cha mguu, iwe rangi ya Dark Blue.
- ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi
- iii. Sweta aina ya Pull Over rangi ya Blue.
- iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu visiwe na nembo na visigino virefu (**Flat Shoes**) vyenye gidamu yaani vya Kamba.
- v. Soksi nyeupe jozi mbili.
- vi. Rangi ya ijabu ifanane na sare za shule.

**b). WAVULANA**

- i. Suruali mbili (2) rangi ya Dark Blue, upana wa chini uwe inch 17, zenyе marinda ya upanga mawilimawili kila upande, mifuko miwili pembedni na nyuma mfuko mmoja (**Modo haziruhusiwi**).

- ii.** Shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi (**zisiwe modo**).
- iii.** Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu visiwe na nembo na visigino virefu (**Flat Shoes**) vyenye gidamu yaani vya Kamba.
- iv.** Sweta aina ya Pull Over rangi ya Blue.
- v.** Soksi nyeupe jozi mbili (2).
- vi.** Mkanda mweusi wa ngozi (**usewe wa tambi**)

### c). SARE ZA MICHEZO

#### **WASICHANA**

- i.** Track Suit rangi ya Blue
- ii.** Raba na soksi za michezo

#### **WAVULANA**

- i.** Jezi za rangi ya Blue
- ii.** Raba na soksi za michezo

### **2.2 MAHITAJI MENGINE**

- ❖ Counter Book kumi na mbili (12) na madaftari makubwa kumi na mbili (12) kwa ajili ya mazoezi mbalimbali.
- ❖ Kalamu mbili (2) na mkebe mmoja wa hesabu (Mathematical Set)
- ❖ Four Figure moja (1).
- ❖ School bag (Sio mfuko wa Plastick)
- ❖ Dictionary (Kamus ya Kiingereza-Kiingereza).

### **3.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyoboreshwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii:-

- a)** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b)** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c)** Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
- d)** Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e)** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f)** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g)** Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i)** Kutunza mali za Umma.

**3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU  
KUSIMAMISHWA SHULE**

- a)** Wizi
- b)** Uasherati na Ushoga
- c)** Ukabaji
- d)** Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika
- e)** Kupigana au kupiga
- f)** Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- g)** Kuwa mjamzito/Kupata mimba
- h)** Kuoa au Kuolewa
- i)** Kutoa mimba
- j)** Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
- k)** Kukataa adhabu kwa makusudi
- l)** Kuwa na simu ya mkononi
- m)** Kumiliki au kukutwa na vitu vyenye ncha kali kama kisu, sindano, pisipisi n.k.
- n)** Kukwepa au kukataa kwa makusudi kufanya mtihani

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA  
KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- a)** Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
- c)** Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**NB:** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAGU**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
THE PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
MAGU DISTRICT COUNCIL**

MAGU SECONDARY SCHOOL,  
P.O.BOX 186,  
MAGU.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**(To be completed by a Medical Officer)**

Pupils full name .....

Age .....

Blood count (red and white)

Stool .....

Urine .....

Syphilis Test .....

T.B Test .....

Eye Test .....

Ears .....

Chest .....

Spleen .....

Abdomen .....

**ANY ADDITIONAL INFORMATION** eg. Physical defects, Chronic or Family diseases, e.t.c

.....  
.....  
.....  
.....

Signature .....

Designation .....

Station .....

Date .....

\*Delete as necessary:

# FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEW

## SEHEMU A: Habari za mwanafunzi (ijazwe na mwanafunzi)

1. Jina kamili .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Wilaya alipozaliwa .....
4. Kukubali nafasi (ijazwe na mwanafunzi)

PICHA  
YA  
MWANAFUNZI

Mimi ..... nimesoma maagizo yote ya kijiunga na shule ya Sekondari Magu na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Magu Sekondari nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata elimu ya kujitegemea.

Sahihi ya Mwanafunzi ..... Tarehe .....

## SEHEMU B: Habari za mzazi/mlezi (Ijazwe na mzazi/mlezi).

1. Jina kamili .....
  2. Yeye ni mzazi/mlezi? .....
  3. Kazi yake .....
  4. Anwani ya mzazi/mlezi .....
- .....  
.....
5. Namba tatu (3) za simu ikiwemo ya mzazi/mlezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi.
    - a) .....
    - b) .....
    - c) .....

## UTHIBITISHO

Mimi mzazi/mlezi wa ..... nimehakikisha kwamba maagizo yote yameelewaka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

Sahihi ya mzazi/mlezi ..... Tarehe .....

**SHULE YA SEKONDARI MAGU**